

inatarajia kujenga masoko ya samaki saba na mialo mitatu

HOJA YA HAJA



TANZANIA imeendelea kutajwa vizuri katika ukuaji wa uchumi kutokana na kasi yake kubwa kupitia sekta mbalimba...



Na SULEIMAN JONGO

Wadau changamkieni fursa hizi katika uvuvi

TANZANIA imeendelea kutajwa vizuri katika ukuaji wa uchumi kutokana na kasi yake kubwa kupitia sekta mbalimbali za uzalishaji mali.

Akiwa nchi Norway, juzi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alisema kwa mwaka 2024 Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), lilisema kuwa Tanzania inatarajia kuwa kati ya nchi 20

Rais Dk. Samia alisema hiyo ni fursa kwa wawekezaji kutoka Norway kuchangamkia nafasi zilizopo nchini kwa kuwa kuna mazingira...

zenye uchumi unaokuwa kwa kasi duniani.

Rais Dk. Samia alisema hiyo ni fursa kwa wawekezaji kutoka Norway kuchangamkia nafasi zilizopo nchini kwa kuwa kuna mazingira mazuri ya kisiasa, kijiografia na kiuchumi.

Moja ya sekta zinazokuwa na kuongeza mchango wake katika ajira, uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa

ujumla, ni uvuvi.

Jitihada na mikakati mbalimbali imeendelea kuwekwa kuhakikisha uvuvi unaimarika na kuwa eneo lenye mchango mkubwa kwa kukuza uchumi.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni ujenzi wa mialo, masoko ya samaki na kuwawezesha wavuvi kuvua kisasa kwa tija zaidi.

Serikali imesema katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, inatarajia kujenga masoko ya samaki saba na mialo mitatu kwa lengo la kuboresha miundombinu ya uvuvi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alipojibu swali la Mbunge wa Nkasi Kusini (CCM), Vicent Mbogo aliyetaka kujua ni lini serikali itajenga masoko ya kuuzia samaki katika kata za Ninde, Wampembe na Kala wilayani Nkasi, Mkoa wa Rukwa.

Mnyeti alisema serikali inaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo

katika mwambao ya Ziwa Tanganyika.

Napongeza mikakati hii inayowekwa na serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambayo matunda yake yameendelea kuonekana.

Moja ya matunda hayo ni kuongeza uwezo wa wavuvi wadogo kuvua kisasa, kuvua samaki wengi kuliko ilivyokuwa awali hatua ambayo inawaongezea tija.

Hata hivyo, bado ipo fursa kubwa ya kuendelea kufanya vizuri na kunufaika zaidi na uvuvi iwapo juhudi hizo za serikali zitapokewa kwa mikono miwili na wadau mbalimbali.

Kwa upande wa wavuvi; ni muhimu wakaendelea kuzingatia hatua muhimu za uvuvi wa kisasa, kujiunga katika vikundi na kuomba mikopo ambayo wataitumia kujiimarisha hatimaye kujiongezea kipato.

Wakati wa kuongeza manufaa ya shughuli za uvuvi ni hivi sasa, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia imedhamiria na inaonyesha kwa vitendo kwamba ipo tayari kuwainua wavuvi, hivyo wachangamkie fursa zinazojitokeza.